JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA 2026

Namba za Simu:
Mkuu wa Shule: 0788424847
Makamu Mkuu wa Shule: 0620788163

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA RUKWA,
S.L.P 229,
SUMBAWANGA.

Tarehe: 18.11.2025

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………………………..
S.L.P …………………………………..…..
…………………………………………..…….

**1. YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA RUKWA, HALMASHAURI YA SUMBAWANGA MKOA RUKWA MWAKA 2026.**

1.Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika Shule hii mwaka 2026.

Shule ya Sekondari ya wasichana ya Rukwa ipo umbali wa Kilometa 95 KUTOKA Mji wa Sumbawanga Barabara ya Kuelekea Mbeya.

Usafiri wa basi kutoka mjini SUMBAWANGA unapatikana katika kituo cha mabasi KATUMBA. Nauli ni Shilingi 5,000/= kwa wanafunzi wanaotokea KIGOMA, TABORA NA KANDA YA ZIWA. Wanafunzi wanaotokea BARABARA YA MBEYA shule ipo mji mdogo wa laela kabla hujafika sumbawanga mjini.

Ukifika LAELA nauli ya kwenda Shule ya sekondari ya wasichana ni Tshs. 1,000/= tu kwa pikipiki. Muhula wa Masomo unaanza tarehe 8/1/2026.

Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 7/1/2026. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 14/1/2026.

2**. Mambo muhimu ya kuzingatia: -**
2.0 Sare za shule

i) Sare ya shule hii ni SKETI mbili (KIJIVU na UGORO) NDEFU HADI KIFUNDO CHA MGUU WAKE na mashati meupe mawili mikono mifupi
.

**Sare ya michezo;** kwa shule hii ni bukta 2 rangi NYEUSI na tracksuit pair moja rangi NYEUSI.
ii) Viatu vya shule vyeusi vya KUFUNGA NA KAMBA vyenye visigino vifupi.
iii) Soksi jozi mbili Nyeupe za shule.
iv) Sweta pair 2 (**UGORO 1 na KIJIVU.1**)

v) Nguo za kushindia (shamba Dress) Gauni drafti ndogondogo damu ya mzee NDEFU KUFIKA KIFUNDO CHA MGUU WAKE na T-shirt ya kola (form six) ya bluu yenye kola nyeupe na ufito mweupe mwishoni mwa mikono

vi) Tai 2 (**KIJIVU 1 na UGORO 1**)

2.1 **Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -**
i.Madaftari counterbooks 9 (3 quire);
ii.Ream za Karatasi $A_4$ Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vyombo vya kulia chakula; container yenye mfuniko rangi ya bluu,kijiko
iv vifaa vya malazi;.**Godoro 1 foot mbili na nusu inchi 4 unene**
.Mashuka Jozi 2 ya pink , blanket 1, , chandarua 1.
vi.Nguo za ndani za kutosha;
vii. **vifaa vya usafi;**.Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko, Jembe 1 na Mfagio 1 laini (soft broom),

**3.0 Sheria na Kanuni muhimu za Shule**:

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.

Hivyo mwanafunzi Anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na atapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

3.**1 Sheria na Kanuni za Shule**
i.Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la **lazima**.;
ii.Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii.Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv.Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v.Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi.Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii.Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii.Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix.Kutunza mali za shule;
x.Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi.Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu ama line ya simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa.**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule.**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kulala kitanda kimoja watu wawili;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki na kukutwa au kutumia simu ya mkononi

xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

xviii. Kwenda nyumba za walimu au wafanyakazi bila kibali maalumu

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i.Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. TAFADHARI PIMA KUPATA UHALISIA WA AFYA YA MTOTO
ii.Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii.Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule

iv. Fomu ya uthibitisho wa Uraia

v.Picha nne (4) za PASSPORT SIZE za Wazazi/walezi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**.
**KARIBUNI SANA.**

Saini ya Mkuu wa Shule:……………………

Jina la Mkuu wa Shule: JANE FRANCISCO KANYAMA

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI WASICHANA RUKWA

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi, hivyo mzazi atume pesa. **TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO**
**USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- Mkuu wa shule: 0788424847
- Makamu Mkuu wa Shule: 0620788163
- Simu ya shule; 0761860548

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
THE PRESIDENT'S OFFICE

RUKWA GIRLS HIGH SCHOOL

P.O. BOX 229,
SUMBAWANGA.

DATE………………………

MEDICAL OFFICER
…………………………………………
…………………………………………
…………………………………………

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR…………………………………
(NAME OF STUDENT)

Please examine the above named as to his/her fitness as indicated below. Arrange the necessary treatment so that the certificate may be brought to school by the student.This certificate must be signed by a qualified Medical Officer of a recognized Government hospital.

1. Hemoglobin ………………………………………………………………………
2. P.V Blooding ……………………………………………………………………..
3. (a) Blooding …………………………………………………………………...
   (b) Hearing ……………………………………………………………………….
4. Blood pressure …………………………………………………………………...
5. Stool for routine examination ………………………………………………...
6. Urine for sugar …………………………………………………………………...
7. Skin diseases ……………………………………………………………………..
8. Leprosy …………………………………………………………………………….
9. Pulmonary tuberculosis ……………………………………………………
10. Asthma …………………………………………………………………………….
11. Epilepsy …………………………………………………………………………..
12. Deformity ………………………………………………………………………
13. Mental problem …………………………………………………………………
14. Comment………………………..………………………………… …………………

Name of medical officer……………………… Signature………………. Date………………

Official stamp

# HISTORIA YA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi……………………………………….……………………………

Jina la baba ……………………………………..…………………………………..

Jina la mama …………………………………..……………………….…………

Shule ya msingi aliyosoma ………………………………………………………..…

Kijiji atokacho ………………………………………… kitongoji cha …………………

Tarehe ya kuzaliwa …….................. Dini …………………Dhehebu …………………..

Kabila …………………………….

**UTHIBITISHO:**

**5.1 Ahadi ya Mwanafunzi**

Mimi ……………………………………………………………… nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha …………… mwaka …………. Katika shule ya Sekondari ya wasichana RUKWA, ninaahidi:-

i. Kuzingatia taratibu na kanuni zote za shule

ii. Kuweka bidii katika masomo yote

iii. Kushiriki katika shughuli za elimu ya kujitegemea

iv. Kuwa na nidhamu ya juu ndani na nje ya shule

**Jina ……………………………………………………………….**

**Sahihi …………………………….……………**

**Tarehe ………………………………...**

**5.2 FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE**

Mimi ……………………………………………… mzazi /mlezi wa …………………………….

Naahidi kwamba:

i. Nitatimiza gharama za mwanangu kama nilivyoelekezwa

ii. Nitamhimiza mwanangu kuzingatia taratibu za shule pamoja na masomo

iii. Nakubaliana na kanuni na sheria zilizotolewa na serikali juu ya mwanafunzi (mwanangu)

iv. Nitatoa ushirikiano kwa walimu endapo mtoto wangu atafanya kinyume na sheria

**Jina …………………………………………………………………**

**Sahihi …………………….………………………**

**Tarehe …………………….……………………...**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MKOA WA …………..………..………………**

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,
Wilaya ya ……………………….
S.L.P ……………………………..
……………………………………

**UTHIBITISHO WA URAIA WA MWANAFUNZI.**

Nathibitisha kuwa……………………………………………….(jina kamili la mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa/kuandikwa Baba yake (Jina kamili) au Mama yake (Jina kamili) ……………………………………………………Amezaliwa katika Mkoa wa………………………………………….Kata ya……………………… tarafa ……………………………. Hapa nchini.

**…………………………………**

**MKUU WA WILAYA**

***NB: kila mwanafunzi analazimika kuishughulikia fomu hii kikamilifu. Ikisha jazwa irudishwe kwa mkuu wa shule tarehe ya kuripoti shuleni.***

# MCHORO NA MFANO WA SKETI YA SHULE

- **NB:** ***Mfano Huu wa sare Uchapishwe Kwa Kwa Rangi ( Print Coloured )***







# MCHORO NA MFANO WA SHAMBA DRESS YA SHULE



**GAUNI LA KAZI/KUSHINDIA (SHAMBA DRESS) ZIWE MBILI**
- Gauni la kazi (Shamba Dress) iwe mshono wa solo
- Rangi Zambarau isiyobana (kifua/mwili kwa ujumla)
-Urefu toka kwenye kisigino hadi kwenye pindo la gauni usizidi sentimeta 18



# MFANO WA T SHITS ZA SHULE

